

HALMASHAURI YA WILAYA YA GAIRO



VIVUTIO NA FURSA ZA UTALII WILAYANI GAIRO



Imeandaliwa na;
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Gairo,
S.L.P 40,
Gairo.

Baruapepe: info@gairo.go.tz

Tovuti: www.gairo.go.tz



Septemba, 2019

1.0 Utangulizi

Sekta ya utalii inakua kwa kasi na ndiyo inayoongoza kuwa katika kuchangiaa pato la taifa ambapo kwa mwaka 2018 ilichangia 25% ya pato ghafi Taifa (Bilioni 4.7). Inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2025 sekta ya Utalii itachangia pato la Taifa kwa Dola za Kimarekani Bilioni 16. Sekta hii ni kichocheo muhimu cha ukuaji wa uchumi kitaifa na kimataifa kwani imeajiri watu wengi sambamba na kutoa mchango mkubwa kiuchumi, kijamii, kisiasa na katika juhudi za kulinda na kuhifadhi mazingira na Baianowai zilizopo. Vivutio vya utalii, miundo mbinu, utulivu wa kisiasa, usalama na huduma zitolewazo katika eneo husika ni vishawishi vikubwa vinavyo wavutia watalii na kuwafanya kutembelea maeneo mbalimbali.

2.0 Miundombinu

Wilaya ya Gairo ina miundombinu inayojitosheleza inayofanya shughuli za utalii kufanyika kwa ubora wa hali ya juu. Miundombinu iliyopo ni pamoja na barabara kuu ya lami itokayo Morogoro kuelekea Dodoma ambapo ndipo makao makuu ya nchi yalipo. Zipo pia barabara za changarawe zinazounganisha vijiji, kata na Wilaya za jirani za Kongwa, Kilindi, Kiteto, Kilosa na Mvomero. Barabara hizi hupitika katika kipindi chote cha mwaka ingawa zipo barabara chache ambazo msimu wa mvua zinapitika kwa tabu kidogo kutokana na utelezi na mito kujaa maji. Aidha, ipo miundo mbinu ya umeme na simu katika maeneo mengi ya mjini na vijijini.

3.0 Huduma za kijamii

Zipo huduma mbalimbali za kijamii zipatikanazo ndani ya Wilaya ya Gairo. Huduma hizo ni pamoja na; huduma za Elimu, Afya, Kifedha, Maji, Hoteli, Umeme na Mawasiliano. Huduma za kifedha zinapatikana katika maeneo ya mjini kwenye benki za CRDB na NMB na vijijini kupitia kampuni za simu kwenye huduma za Airtel Money, M Pesa, Tigo Pesa na Halo Pesa nk. Huduma za Afya zinapatikana maeneo yote ya vijijini kupitia Zahanati na Mjini kwenye kituo cha Afya Gairo. Huduma za afya zinatarajiwa kupatikana pia katika Hospitali ya Wilaya siku za karibuni kwani ujenzi wake upo katika hatua za ukamilishwaji. Huduma za malazi na chakula zinatolewa na serikali (Camping site ndani ya maeneo ya hifadhi) pamoja na sekta binafsi kwenye Hoteli na Nyumba za kulala wageni zikiwemo; MC Lodge, Moleti Lodge, Kadudu Lodge, Rubeho Lodge, Diana Lodge, Msela Lodge, Aljazeera Hotel na Mama Lishe waliopo katika maeneo mbalimbali. Pia lipo soko la kila

siku katikati ya Mji na minada (Magulio) mbalimbali kama mnada wa Msasani, Rubeho na Ukwamani/soko la mahindi ifanyikayo mara moja kwa juma. Aidha, bado zipo fursa nyingi za uwekezaji katika sekta ya utalii hususani katika ujenzi wa Hoteli, Nyumba za kulala wageni na Kampuni za kupokea na kusafirisha watalii (Tour Operators & Travel Company).

4.0 Vivutio vya utalii vilivyopo Wilayani Gairo

4.1 Milima ya Ukaguru inayounda Safu za Milima ya Tao la Mashariki (Eastern Arc Mountain)

Jiografia ya Gairo imegawanyika katika uwanda wa tambarare na uwanda wa juu (milimani) ambao umetawaliwa na safu za milima ya Ukaguru ambayo ni sehemu ya safu za milima ya Tao la Mashariki (Eastern Arc Mountains). Sehemu kubwa ya milima hii ni Hifadhi za Misitu ya Taifa (Hifadhi za Taifa za Mamiwa kaskazini na Ikwamba pamoja na shamba la miti la serikali Ukaguru). Misitu hii ina ndege wa zaidi ya aina 60 wakiwemo ndege adimu duniani ambao ni; Rubeho Warbler (Endemic spp.), Moreaus sunbirds, Lubeck warbler, Lubeck akalat, African tailorbird na Olive flanked robin pamoja na wanyama wadogowadogo kama vile Nyani, Kima, Komba, Ngedere, Tumbili, Galago (Bush baby), Panya, Vyura filimbi (*Anthroleptis nikeae*), vinyonga wenye pembe tatu, vipepeo na mmea adimu aina ya *Lobelia sancta* (Endemic spp), *Macaranga capensis*, *Impatiens ukaguruensis* (Endemic) na *Streptocarpus Schlieberii*. Aidha, zipo hifadhi za misitu ya vijiji kwenye uwanda wa tambarare ikwemo hifadhi maarufu ya miti hadimu ya Mipingo ijulikanayo kama Leshata Vipigo Forest Reserve) uliopo katika kijiji cha Leshata.



Picha: Ikionyesha Hifadhi ya Msitu Taifa wa Asili wa Mamiwa Kaskazini



Picha: Ikionyesha ndege hadimu aitwae Rubeho Warbler



Picha: Ikionyesha ndege hadimu aitwae Moreaus sunbirds

Katika Hifadhi ya Taifa ya Msitu wa Mamiwa Kaskazini wapo pia vyura waitwao Chura filimbi (*Anthroleptis nikeae*). Jina hili la Chura filimbi limetokana na wao kulia kwa kutoa sauti kama filimbi. Vyura hawa hupatikana katika eneo hili pekee na wanaurefu wa 54.04mm and 55.82mm. Hupenda kuishi kwenye majani makavu ya miti yaliyodondoka na chakula chao ni wadudu wadogowadogo kama vile mchwa na sisimizi.



Picha: Ikionyesha Chura adimu Duniani aitwae Chura Filimbi (*Anthroleptis nikeae*)

4.2 Maporomoko ya maji na Mapango ya Ukaguru

Katika Shamba la Miti Ukaguru yapo maporomoko ya maji yenye urefu wa mita 27 yajulikanayo kama **"Ukaguru Waterfall"** na Pango lenye sehemu nne (4) lililopo jirani na maporomoko haya. Wajerumani walikuwa wakijificha katika Pango hili ili kujihami

dhidi ya maadui. Watalii wengi hutembelea eneo hili ili kuona na kufurahia madhari iliyopo.



Picha: ikionyesha maporomoko ya maji ya Ukaguru yaliyopo katika Shamba la Miti Ukaguru.



Picha: Ikionyesha Hifadhi ya Msitu wa Mipingo Leshata (Leshata Vipigo Forest).

4.3 Majengo na Magofu ya Kale.

Katika Wilaya ya Gairo yapo majengo na magofu ya kale ambayo ni ya kiistoria yakiwemo; majengo ya Mahakama ya mwanzo ya Idibo (1938 - Mjerumani), Mahakama mwanzo Nongwe (1954 - Waingereza), Shule ya msingi Kisitwi (1935) na Magofu ya kale ya Rubeho (1934 - Thomas Baine). Majengo na Magofu haya ni kielelezo kuwa; wakoloni waliishi katika eneo hili miaka mingi iliyopita wakifanya shughuli mbalimbali za kibinadamu ikiwemo kilimo na uchimbaji madini.



Picha: ikionyesha jengo la Mahakama ya Mwanzo Idibo lililojengwa mwaka 1938



Picha: ikionyesha jengo la Mahakama ya Mwanzo Nongwe iliyojengwa mwaka 1954



Picha: ikionyesha jengo la Shule ya Msingi Kisitwi iliyojengwa mwaka 1936.



Picha: ikionyesha Magofu ya kale ya Rubeho yaliyojengwa na mkoloni Ngudu Thomas Baine mwaka 1934

4.4 Jiwe la Mungu

Katika kijiji cha Muheza Ititu lipo jiwe kubwa la kuvutia lijulikanalo kama **Jiwe la Mungu** linalokadiriwa kuwa na uzito wa tani 7 ambalo lipo juu ya udongo wenye upana wa mita 2 na kimo cha mita 16.3. Jiwe hili limekuwa kivutio kikubwa kwa watalii wengi kutokana na mwonekano wake na manzari nzuri ya eneo lilipo.



Picha: Ikionyesha muonekano wa jiwe la Mungu katika kijiji cha Muheza Ititu

4.5 Alama za Nyayo zinazosadikiwa kuwa za wanadamu wa kale juu ya mwamba na jiwe katika vijiji vya Nguyami na Muheza Ititu

Uwepo wa alama zinazosadikiwa kuwa ni za nyayo za wanadamu wa kale juu mwamba na jiwe katika vijiji vya Nguyami na Muheza Ititu vinafanya Wilaya ya Gairo kuwa sehemu muhimu katika kutafuta chimbuko la mwanadamu. Watalii wengi hutembelea maeneo haya ili kuona, kufurahia na kujifunza mambo mbalimbali juu ya chimbuko la mwanadamu.



Picha: ikionyesha alama inayosadikwa kuwa unyayo wa mwanadamu wa kale katika kijiji cha Muheza Ititu



Picha: Ikionyesha alama ya unyayo wa mwanadamu wa kale katika kijiji cha Nguyami

4.6 Hifadhi ya Mlima Gairo

Katika eneo la Mji wa Gairo ipo Hifadhi ya Mlima Gairo ambayo hutembelewa na watalii kwa ajili ya utalii wa kupanda milima na upigaji wa picha. Jina la mji wa Gairo limetokana na jina la mlima huu ambao zamani ulijulikana kama **"Igawiro"** maana yake ni **"Sehemu ya kugawana mali"**. Wenyeji (Wakaguru) walikua wakitumia eneo hili kama sehemu ya kugawana mifugo na nyama baada ya uwindaji. Aidha, wenyeji wa Wilaya hii hutumia sehemu ya kilele cha mlima huu kwa ajili ya ibada za kimila na matambiko. Uwapo katika kilele cha mlima huu utapata fursa ya kuuona Mji wa Gairo na maeneo ya jirani kama vile Chakwale, Kibedya, Mtumbatu, Panda mbili na Mlali. Mipango tulionayo ni kuanzisha utalii wa kuruka kwa maparachuti (Balloon) kutoka katika kilele cha mlima huu katika siku za mbeleni.



Picha: ikionyesha sehemu ya kilele cha Hifadhi ya Mlima Gairo na madhari ya Mji wa Gairo.

4.7 Utawala wa Kichifu

Wenyeji wa Wilaya ya Gairo ni kabila la Wakaguru ambao katika utawala wa jadi na mila walikuwa chini ya utawala wa Chifu Mgego Sekwao Said aliezaliwa 1841 na kufariki mwaka 1946. Chifu Sekwao alitawala mwaka 1900 – 1940 na baadae alirithiwa na mwanae aitwae Chifu Isaya Said Sekwao aliyetawala kuanzia mwaka 1940-1973 na baadaye kurithiwa mdogo wake aitwae Chifu Mndewachaka Sekwao kuanzia mwaka 1973 hadi sasa. Gairo ni miongoni mwa Wilaya ambazo jamii na watu wake wanaheshimu sana taratibu za mila na desturi. Jamii hii imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutunza, kulinda na kuheshimu utamaduni wao. Chifu wa kabila la Wakaguru ndiye msimamizi mkuu wa masuala ya mila na tamaduni.



Picha: ikionyesha Kaburi la Chifu Mgego Sekwao Said



Picha: ikionyesha Boma la Chifu wa sasa aitwae Mndewachaka Sekwao.

5.0 Njia za kupita watalii (Tourist Trail/Circuit)

Zipo njia tatu zitumiwazo na watalii zinazowawezesha kufika katika maeneo mbalimbali ili kujionea vivutio vya utalii vilivyopo. Njia hizo ni;

- Gairo – Mlima Gairo – Gairo.
- Gairo – Muheza Ititu – Gairo, na
- Gairo – Hifadhi ya Taifa ya Msitu wa Mamiwa Kaskazini – Gairo.
- Gairo – Nguyami - Gairo

Vivutio vyote vilivyopo vinafikika kwa Gari isipokuwa baadhi ya maeneo ambapo huwalazimu watalii kutembea kwa miguu. Mfano kupanda katika kilele cha mlima Gairo. Aidha, wapo waongoza watalii (Tour Guide) waadilifu na wenye ujuzi wa kutosha jambo ambalo huwahakikishia watalii usalama watembeleapo vivutio vyetu.

"Karibu Gairo ufurahie Vivutio vitakavyo kufanya kurejea tena na tena"